

MAKALA

Vifaranga vya nje vinavyoua soko la wawekezaji wa ndani

Na Mwandishi Wetu

KATI ya sekta ambazo zinaweza kuingizia serikali mapato ya uhakika ni pamoja na sekta ya mifugo, kutokana na kwamba ni kitowenio kinacholiwa na watu wengi kuanzia vijiji hadi mijini.

Mapato hayo yanaweza kuwa kwa njia ya uwekezaji kwenye uzalishaji wa vifaranga nchini, na kwamba wawekezaji wa ndani ya nchi wanaweza kuzalisha vifaranga na kuza kwa wafugaji wa kuku amba nao wanakuwa na jukumu la kukuza vifaranga na vikilikuwa vinauzwa kama kuku kwa ajili ya chakula.

Licha ya uhalisia huo sekta hiyo inakabiliwa na wakati mgumu kutokana na soko kufurika vifaranga kutoka nje ya nchi, halii inayowafanya wazalishaji wa ndani kushindwa kushindana kwa sababu ya bei na gharara za uwekezaji walizonazo.

Katika kulinda soko la ndani wazalishaji, wafugaji na wauzaji wa vifaranga wa kuku wa nyama wameombwa serikali kusitisisha uingizaji wa vifaranga hivyo kutoka nje ya nchi.

HALI IKOJE

Ufutuiliaji wa gazeti hili umebaini kuwa kuna tatizo katika udhibiti wa magendo ya uingizwaji wa vifaranga nchini ambapo vifaranga kutoka nchi za Uganda na Malawi vimekuwa vikiingia kimagendo.

Vifaranga kutoka nje ya nchi vikiingizwa hapa nchini vinauzwa kwa bei ya chini zaidi na hivyo kwa wazalishaji na wauzaji wa ndani wanajikuta wakikosha soko la kuuza vifaranga vya, hatua inayopelekea wengine kuishia kubakia navyo ndani.

Kabla ya kukithiri kwa uingizwaji wa vifaranga kwa njia za magendo mfanyakishashara, wa kati wa vifaranga anayenunua kwa wazalishaji wa ndani alikuwa anauza boksi 50 zenye vifaranga 5,000 vya kuku, lakini kwa sasa hatua hiyo imekuwa ngumu kufikila na kujikuta akiuza boksi tano kwa mwezi hatua inayomrudisha nyuma kimaisha.

Mfanyakishashara ya kuku wa Kimara, Haruna Hamza anaililia serikali kuanza kuchukua hatua dhidi ya uingizwaji wa vifaranga kimagendo huku akitaka kuweka msisitizo katika kauli aliyoita ya kusitisisha vibali vya kuingiza vifaranga nchini.

Anasema licha ya uingizwaji wa vifaranga kwa njia za magendo lakini bado wizara ya mifugo imetoo vibali kwa kampuni kadhaa kuingiza vifaranga ambapo waingizaji hao wanachangia kuua soko la ndani.

Rais Samia Suluhu Hassan anayo ni ya dhati ya kulinda soko la ndani ya uzalishaji wa vifaranga ambapo



na siye tunanunuwa kwa wazalishaji kisha kuza kwa wafugaji mitaani, sasa kama wakiendelea kuwepo wanaoingiza kutoka nje ya nchi na kuza kwa bei ndogo kwa wafugaji hao hao, ni wazi kuwa siyo tunaonunuwa kwa wazalishaji wa ndani wote siye na wazalishaji wenye wibashara zinaenda kufa," anasema na kuonegeza:

"Nilikuwa naufuga na kuza kuku 3,600 kwa mwezi, ila kwa sasa hata 1,000 hawafiki na mtaji unaendelea kukata kwa hapa naona kunahitajika rijadala wa kina kwa kweli katika nje ya wazalishaji wa ndani na serikali."

Salima Msangi mkazi wa Gongo la Mboto anasema "Juji nimeuza kuku mmoja kwa Sh.4,000 ni hasara sana, wakiendelea kukaa ni hasara ni bora niuze kwa hasara, soko limejaa vifaranga na kuku wengi sana, hii haina afya kwa uchumi wetu ni lazima serikali ili galie kwa jicho la pekee."

Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji wa Kuku wa Nyama Tanzania (TABROFA), Aloyce Makoye anasema kama hakutakwa na hatua za haraka za kusaidia wawekezaji wa ndani dhidi ya vifaranga kutoka nje ya nchi, blashara ya ndani inaenda kufa.

"Mbali na kuingizwa kwa vifaranga kutoka nje kuathiri soko la ndani lakini bado kuna wingi wa kuku wa nyama wanaoingizwa sokoni kutoka nje sasa matokeo yake wazalishaji wa vifaranga wa ndani wanapata

shida huku hata kwenye soko wauzaji wa kuku nao wakikumbana na changamoto," anasema Makoye.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti huyo, halii hii tete hajjawahi kutokea katika biashara ya kuku wa nyama kwa kampuni zote kulalama biashara ni ngumu.

"Ukienda Interchick, Kibo, Organia, Alvin na wengine wanalamika biashara ni ngumu, hivyo nashauri miyaka iangaliwe, kwani tunapoenda ni pabaya na vibali vya kuingiza vifaranga kutoka nje visitolewe, ili hizi kampuni za ndani ziwe na uhakika wa soko na

hivyo zizalisha kwa wingi hatua itakayowanufaisha wauzaji vifaranga wadogo wa ndani."

Mkurugenzi wa Kampuni ya Kuzalisha Vifaranga ya Organia, Albert Momdjian anasema kampuni hiyo ikiwa kama katika nje ya wazalishaji wa ndani pamoa na mawakala wao wanauuza vifaranga vya wameathiriwa kwa kiasi kikubwa na uingizwaji wa vifaranga kutoka nje.

Anasema kwa sasa kampuni hiyo inaingia hasara katika undeshwaji wa shughuli zake hapa nchini kwa kuwa

wanunuzi wamepungua kutokana na wengi wao kununua vifaranga vikiwemo vinavyoingizwa kimagendo kutoka nje ya nchi.

"Wadau wa uwekezaji wa bisashara ya vifaranga hasa tunazalisha hapa nchini tuliambiwa kuwa hakuna vibali vipywa vinyotolewa kwa kampuni za kuingiza vifaranga na kuwa kampuni zilizopewa vibali vyo vinatataka wa hadi sasa view vimeshaista muda wake wa kazi," anasema Momdjian.

KAULI YA SERIKALI

Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo ambaye pia ni Mto Vibali vya kuingiza mifugo ikiwemo vifaranga, Prof. Hezron Nonga wa Wizara ya Mifugo na Uvuuvi, anasema serikali hajatoa vibali vipywa vya uingizaji vifaranga nchini na kuwataka wanaojuu njia za panya wajulishere serikali.

Anasema hadi sasa kampuni zinazoingiza vifaranga ni mbili ambazo ni Wolowolo Animal Care Center na The One Agro Enterprise ambazo zilipata vibali kuanzia mwaka janja na kwamba vifaranga vinyoingizwa ni katika kumaliza maombi yao ya zamani.

"Hizi kampuni ziliomba vibali katika kipindi ambacho nchi ili-kuwa na changamoto ya uhaba wa vifaranga ambapo The One Agro Enterprise imeruhusiwa kuingiza vifaranga 494,000 kutoka Uganda na Wolowolo vifaranga 150,000 kutoka Malawi na mwisho wakuingiza ni Januari 15,2023," alisema.



lugha huyo katika mataita
mbalimbali.
"Tunapoadhimisha

ya kutundisha Lugha ya
Kiswahili katika nyanja na
nchi mbalimbali.

"ipauayo.....
makubaliano na itasaini-
wa," alisema.

katika eneo ulimwengu.....
zao la mwani na viwanda.

*'Ng'ombe wa maziwa wanalipa'

HABARI LEO UK 4

Na Ally Ruambo

WATANZANIA wametakiwa kuwekeza katika shughuli za ufugaji wa ng'ombe wa maziwa kwani biashara hiyo ina faida na sasa imefikia thamani ya dola za Marekani milioni 1.28.

Wito huo ultirolewa na Msajili wa Bodi ya Maziwa, George Msalya alipozungumza katika kilele cha siku maalumu ya unywaji maziwa iliyofanyika katika ukumbi wa Rashid Kawawa uliopo katika Viwanja vya Sabasaba

mkoani Dar es Salaam.

Msalya alisema mpaka sasa kuna jumla ya viwanda 108 vya kusindika maziwa nchi nzima na jitihada zinaendelea kuhakikisha vinaongezeka zaidi ili kuleta tija kwa wafugaji kwa kuuza zaidi bidhaa ya maziwa.

Alisema serikali imejithidi kuhakikisha maziwa yanayosindikwa katika viwanda vya ndani yanakuwa na ubora na kwa sasa yana uwezo wa kuuzwa kokote, hivyo aliwataka wananchi kuunga mkono jitihada hizo kwa kununua maziwa kutoka viwanda vya ndani ili kukuza

uchumi wa taifa.

Aidha, aliwataka wasindikaji wa maziwa kuacha kutumia chupa ambazo zilishatumika kuhifadhi vinywaji vingine kutumia katika matumizi yao na kuwataka kununua vifungashio maalumu ambavyo vinatengenezwa kwa ajili ya biashara hiyo.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega aliishukuru serikali kwa kuendelea kuboresha sekta ya mifugo kwa kutoa fedha ambazo zimevezesha kununua ng'ombe wa kisasa zaidi ya

1,000 wa maziwa na nyama ambaao watagawiwa kwa vikundi na watu binafsi ili kubadilisha aina ya ng'ombe waliopo sasa.

Ulega alisema pia serikali imetoa fedha kwa ajili ya kujenga vituo vya kukusanya maziwa na kwa kuanza vitajengwa katika halmashauri 10.

Aliwataka wakurugenzi wa halmashauri kuvisaidia vikundi vya wanawake na wasindikaji maziwa kupata vifungashio maalumu kwa ajili ya bidhaa zao ili ziweze kutumika shulenii pamoja na sehemu zingine zenyehitaji.